**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA**

**KUMB.NA.LDC/L,10/12VOL. VI/31** **17/12/2025**

## TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA MWENYEKITI WA BODI YA AJIRA

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa anawatangazia Watanzania wenye sifa na nia ya kufanya kazi katika Halmashsuri hii kuomba nafasi ya kazi **ya Mwenyekiti wa Bodi ya Ajira** kwa kipindi cha **Miaka Mitano (5)** kama ifuatavyo:-

### 1.1 MAJUKUMU YA KAZI

i. Kuendesha/kuongoza vikao vya usaili wa waombaji wa nafasi za kazi.

ii. Kuendesha/kuongoza vikao vya kuthibitisha kazini watumishi

iii. Kuendesha/kuongoza vikao vya kupandisha/kuwabadilisha watumishi vyeo.

### 1.1.1 SIFA YA MWOMBAJI

i. Awe Raia wa Tanzania

ii. Awe Mkazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa.

iii. Awe hajawahi kushtakiwa na kosa lolote la Jinai

iv. Awe na Umri wa kuanzia miaka 50 hadi 65

v. Awe na Elimu ya Kidato cha nne au kidato cha sita

vi. Awe na Taaluma ya kuanzia Shahada/Stashahada ya juu katika fani Utawala au Usimamizi wa Rasilimaliwatu.

vii. Awe na weledi katika masuala ya sheria, Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu (Akiwa Mstaafu wa Utumishi wa Umma atapewa kipaumbele).

viii. Awe na Uzoefu katika masuala ya Ajira.

### 1.1.2 POSHO

Kazi hii haina Mshahara wa kila mwezi, Mwenyekiti wa Bodi ya Ajira atakuwa analipwa posho kutokana na vikao vitakavyokaliwa na Bodi.

### 1.1.3 MASHARTI YA JUMLA

i. Mwombaji aambatanishe Wasifu wake kwenye barua yake ya maombi
ii. Mwombaji aambatanishe nakala halisi ya vyeti vyake vya elimu na taaluma
iii. Mwombaji aambatanishe picha 2 za pasipoti katika maombi yake.

**MUHIMU:** Maombi yote yatumwe kwa njia ya Posta kuanzia tarehe**17/12/2025** hadi tarehe **02/01/2026** saa 9:00 Alasiri.

Maombi yaelekezwe kupitia Anwani ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa ifuatayo;-

**Mkurugenzi Mtendaji (W),**
**Halmashauri ya Ludewa,**
**S. L . P. 19,**
**LUDEWA.**

Tangazo hili linapatikana pia katika tovuti ya Halmashauri (*www.ludewadc.go.tz*).

Limetolewa na;

Sunday N. Deogratias
**MKURUGENZI MTENDAJI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA**